**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

# BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI

## TAARIFA KWA UMMA

### ORODHA YA MAJINA NA MADENI YA WANACHAMA WOTE WA PSPTB

**Dodoma Septemba 17, 2026.**

Bodi ya wataalamu wa ununuzi na ugavi (PSPTB) ni taasisi ya serikali iliyopo chini ya Wizara ya Fedha, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya PSPTB Sura ya 179 ya Sheria za Tanzania. PSPTB, ni chombo cha kisheria chenye mamlaka ya kusimamia na kudhibiti viwango, mwenendo na maadili ya taaluma ya ununuzi na ugavi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7(g) cha Sheria ya PSPTB, Bodi hii imepewa mamlaka ya kipekee ya kusajili watu waliokidhi vigezo na kuwapa mamlaka ya kisheria ya kufanya kazi kama Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.

Pia kwa mujibu wa kanuni ya 38(1)(b) ya kanuni za PSPTB, 2009, PSPTB ina mamlaka ya kumfutia mtu yeyote ambae atakuwa hajalipa ada ndani ya miezi 24. Kutokana na hilo tunapenda kuutaarifu umma kuwa tumeweka orodha ya majina na madeni ya wanachama wote wa PSPTB kulingana na ngazi ya usajili kwenye tovuti ya PSPTB na hivyo basi, kila mwanachama mwenye deni anatakiwa kukamilisha malipo ya deni lake kabla ya tarehe 15 Octoba, 2026. Baada ya tarehe hiyo taratibu za kufuta wanachama zitafuata kwa mujibu wa kanuni tajwa vikiwa pamoja na sheria za PSPTB. Tunapenda kukukumbusha kuwa baada ya tarehe tajwa tutatoa orodha ya majina ya wanachama hai (**active members**) wa PSPTB ambao kisheria ndio watastahili kufanya kazi za ununuzi na Ugavi.

Kwa yeyote atakayepata changamoto kuhusiana na deni lake, tafadhali awasiliane na idara ya Uhasibu PSPTB kwa simu namba **0737157312**.

**Imetolewa na :**

Digitally Signed By GODFRED MBANY
Thu Sep 17 15:24:36 EAT 2026

GODFRED MBANYI
**MKURUGENZI MTENDAJI**